THE SALVATION ARMY INTERNATIONAL

# Ujumbe wa Jenerali wa Krismasi ya mwaka 2023

Mwonekano ulikuwa unaojulikana.  Mtaa uliojaa taa za sherehe na mapambo, muziki ukichezwa na umati wa watu wakitembea, wakizingatia  mambo ya Krismasi. Huko mwishoni palikuwepo nyumba ambayo ilikuwa na giza kiasi, ikiwa na boksi dogo lililokuwa na mwonekano wa asili mbele ya uwanja. Watu wengi hata hawakujisumbua kuangalia.  Kwa urahisi onyesho la Krismasi lilimalizika kabla hawajaifikia ile nyumba. Lakini hapo hapo palikuwa na uwakilishi wa kuonekana wa moyo mtulivu wa Krismasi. Sio onyesho lililopangwa kuvutia.  Sio mataa na sauti nyingi.  Bali mtazamo makini na mtulivu juu ya yeye aliyezaliwa kuwa Mwokozi wetu.

Wakati mwingine mimi hushangaa kama inaweza kuwa rahisi kwetu kuukosa moyo mtulivu wa Krismasi.  Hata tunapokuwa tunatazama sehemu ya hadithi ya Krismasi tunaweza tukakosa ujumbe wa msingi wa hayo yote. Kila mwandishi wa injili anaiwakilisha Krismasi kwa njia tofauti. Wengine wanaweza kusema kwamba ni Mathayo na Luka tu ndiyo wanaoingiza hadithi ya Krismasi. Lakini nataka kupendekeza kwamba kila injili inaleta msisitizo wa aina yake.

*Marko* –inawezekana ndiyo injili ya zamani zaidi – hana hadithi ya kuzaliwa au ya utoto. Badala yake, ‘Krismasi’ ya Marko imebebwa katika maneno  ya ufunguzi, ‘Mwanzo wa Injili ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu’ (Marko 1:1). Yesu anaonyeshwa kuwa ni Mwana wa Mungu kutoka mwanzo kabisa. Hiyo ndiyo habari njema.

*Yohana* vile vile hana hadithi ya kuzaliwa wala ya utoto, bali anaonyesha msingi wa Krismasi unatokana na moyo wa Mungu. Neno lililofanyika mwili linaishi katikati yetu – likiwa limejaa neema na kweli.

*Mathayo* anafungua akiwa na orodha ndefu ya majina katika mti wa famila ya Yesu. Ni rahisi kuruka haya na kukosa umuhimu wake. Ndani mna wanawake wa tano ambao wote walionyesha imani ya kipekee, licha ya kwamba jamii ile inaweza kuwa iliwahukumu vikali. Tamari – aliyemdanganya baba mkwe wake kuwa ni mja mzito; Rahabu – kahaba aliyewasaidia wapelelezi Waisraeli; Ruth – mgeni aliyedharauliwa; Bersheba – mzinzi; na Mariamu – mama ambaye hakuolewa. Kila mmoja alikuwa sehemu ya historia ya familia ya Yesu.  Kama Yesu baadaye alionyeshwa kuwa anayeelewana na wenye dhambi, ni kwa sababu imo ‘ndani ya vinasaba vyake’. Yesu anaungana na watu kama sisi ambao – licha ya dhambi na ubinadamu dhaifu – twaonyesha imani. Kisha *Mathayo* anaungana na Yesu akiwa Imanueli – Mungu pamoja nasi, katika ubinadamu wetu.  Yote haya yanafanyika *kabla* ya wale watu wa asili wa Krismasi - Mamajusi  -  hata wajajitokeza.  Wanakuja kumtafuta yeye aliyezaliwa kuwa Mfalme.

*Luka* ana malaika wanaotangaza kwamba Yesu ni Mwokozi, Kristo Bwana. Hii haitolewi kwa watu ambao ungetegemea, bali kwa wachungaji – mara nyingi wanahesabiwa kidini kuwa waliofukuzwa kwa sababu ya aina ya kazi yao.  Kwa watu kama hawa, wanaoishi pembezoni mwa jamii, Yesu anakuja kwao kama Mwokozi.

Kila moja ya injili inatoa mtazamo tofauti wa Krismasi. Ni rahisi kwetu kujishughulisha na  matawi ya hadithi ya Krismasi.  Hiyo inaweza kujumuisha vitu ambavyo tumevizoea, ambavyo hata havijatajwa, ambavyo hata havitajwi katika injili yoyote. Badala yake wakati fulani tunaweza tukaukosa ule moyo mtulivu wa Krismasi ilio sawa na Maandiko.

Mwaka huu, labda tunaweza kuzingatia tena kuhusu nini injili zinatuambia juu ya kuja kwa Yesu. Yeye ajaye kwa sababu ya wenye dhambi na waliotengwa. Yeye ajaye kuwa Mfalme.  Yeye ajaye wa milele.

Pamoja na mambo yote mengine yanayofanyika wakati huu wa mwaka, naomba tuelekeze mioyo na nia zetu kwenye moyo mtulivu wa Krismasi: ukweli wa Yesu ni nani.  Mwana wa Mungu. Neno la uzima lililofanyika mwili. Mfalme wetu. Imanueli. Mwokozi wetu. Kristo Bwana.

Na mwandishi wa wimbo, tunasema ‘Njoo kwetu, kaa nasi, Bwana wetu Imanueli.’

Naomba Mungu akubariki wakati huu wa Krismasi na kote katika mwaka mpya ujao.

**Lyndon Buckingham**
Jenerali